

1.a) Uhakiki wa kazi za fasihi huegemea nadharia bora miengoni mwa nyingi zilizopo. Fafanua kwa tafsili vigezo vyovyote vitano vya ubora huu kuzingatia fasihi ya Kiswahili.

(Alama 15)

b) Jadili dhima ya uhakiki kama dira mwafaka katika uwanja wa fasihi. (Alama 15)

2. Hakiki maudhui yoyote matano yanayowasilishwa katika mojawapo ya kazi za fasihi zifuatazo.

i. *Sauti ya Dhiki* (A. Abdalla)

ii. *Siku Njema* (K. Walibora)

iii. *Amezidi* (S.A. Mohamed)

(Alama 20)

3. Udhanaishi wa Kiafrika unajidhihirisha katika kazi za Euphrase Kezilahabi. Tathmini kauli hii kwa kurejelea kazi zozote mbili. (Alama 20)

4. Kwa kurejelea tamthilia ya *Kilio cha Haki* (Alamin Mazrui) na riwaya ya *Kiza Katika Nuru* (S. A. Mohammed) jadili namna mihimili yoyote mitano ya uhalisia wa kijamaa inavyodhihirika. (Alama 20)

5. Urasimi Mpya unaweza kutumika kuihakiki kazi ya fasihi ya Kiswahili. Eleza kauli hii. (Alama 20)

6. Fasihi ya Kiswahili karne ya ishirini na moja ni ya Kifeministi. Thibitisha kwa kuzingatia *Mama Ee* (Ari Katini Mwachofi) au *Nakuruto* (Clara Momanyi). (Alama 20)